**Tangazo la Serikali Na..... la Tarehe .............**

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI) SURA YA 288

---

**SHERIA NDOGO**

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89(1))*

## SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA UDHIBITI TAKA) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM, MWAKA 2019

### SEHEMU YA KWANZA
### UTANGULIZI

Jina na Tarehe ya kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Utunzaji wa Mazingira na Udhibiti Taka) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2019, na zitatumika katika eneo la Utawala la Jiji la Dar es Salaam baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi maneno haya yatakuwa na maana zifuatazo isipokuwa pale yatakapotumika vinginevyo:-

"*Afisa Mwidhiniwa*" Maana yake ni Afisa yeyote wa Serikali atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"*Baraza*" Maana yake ni Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

"*Jiji*" Maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

"*Kiambaza*" Maana yake ni sakafu imara ya mawe au matofali ya saruji au matofali ya udongo yaliyochomwa na kujengewa kutoka kwenye nyumba hadi kwenye mfereji wa barabara.

"*Mamlaka*" Maana yake ni Eneo la utawala la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

"*Manispaa*" Maana yake ni Manispaa zote za Mkoa wa Dar es salaam zinazounda Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam.

"*Mkurugenzi*" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji

la Dar es salaam au mtu yeyote alikayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"*Mmiliki*" Maana yake ni mtu, kampuni au taasisi yoyote yenye eneo la kuhifadhi taka za aina zote.

"*Taka*" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria za Afya ya Umma ya Mwaka 2009 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004.

"*Uzoaji na Utupaji Taka Ngumu*" Maana yake ni ukusanyaji na uondoaji wa taka zote zinazozalishwa na familia, Kampuni, Sehemu ya biashara, Taasisi na kuzipeleka kwenye vituo vidogo vya taka au kwenye dampo kuu.

"*Wakala*" Maana yake ni Kampuni yoyote itakayoteuliwa kutekeleza shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa Taka au shughuli nyingine zozote zinazohusiana na na ukusanyaji na uzoaji wa taka katika maeneo ya Jiji kwa niaba ya Halmashuri.

## SEHEMU YA PILI
## UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Bustani na upandaji wa miti

3. (1) Halmashauri kwa kushirikiana na Manispaa itaratibu shughuli za upandaji wa miti na utunzaji wa Bustani katika maeneo wazi, kingo za barabara na maeneo mengine ili kuweka mandhari nzuri ya kupendezesha Jiji.

(2) Kila Mmiliki wa Ardhi au Nyumba au Jengo atawajibika kupanda Miti na kuitunza katika eneo lake au kuzunguka nyumba yake kwa ajili ya utunzaji wa mazingira na mandhari.

(3) Ni marufuku kukatiza katika bustani kwa kukanyaga maua au majani au kukata Mti au kuweka matangazo ya aina yeyote, au kuudhuru mti kwa namna yeyote bila kibali cha Halmshauri.

Idadi ya miti ya kupanda kwa kila Mmiliki

4. Kila Mmiliki wa ardhi au Nyumba au Jengo atalazimika kupanda;

(a) Miti isiyopungua sita (6) kwa Mmiliki wa ardhi yenye ujazo chini au kati *(Low and medium density);*

(b) Miti isiyopungua miwili (2) kwa Mmiliki wa ardhi yenye ujazo wa chini *(High density);*

(c) Kila Mmilki wa ardhi au nyumba au jengo atapaswa kupendezesha na kutunza bustani ya maua ili kuwa na madhari nzuri katika eneo lake.

Usafi wa mifereji na njia za waenda kwa miguu.

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki au mpangaji wa Ardhi au Nyumba kuondoa uchafu, mchanga, majani, nyasi na vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mifereji ya maji ya mvua inayozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake.

Usafi na Utunzaji wa Fukwe

6. (1) Halmashauri kwa kushirikiana na Manispaa zitawajibika kutunza na kusafisha fukwe zilizopo ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

(2) Mtu yoyote hataruhusiwa kufanya shughuli za biashara katika maeneo ya fukwe bila kibali cha Halmashauri.

(3) Mmiliki wa nyumba au hoteli iliyo karibu na fukwe hataruhusiwa kutiririsha maji machafu au kutupa taka ya aina yoyote katika maeneo ya fukwe au Baharini.

Utiririshaji wa maji Taka

7. Mtu yeyote hataruhusiwa kuacha wazi shimo la maji taka, choo, karo, "*septic tank*" *Soakage pit*" na "*Cesspool*" au kumwaga maji taka au kutapisha choo au karo kuelekea sehemu isiyoruhusiwa.

Udhibiti wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

8. Itakuwa ni marufuku kwa Mtu yeyote;

(a) Kutelekeza, kuacha gari bovu au mitambo mibovu au vyuma chakavu au kitu chochote ambacho kinasababisha uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya barabara au maeneo yasiyoruhusiwa;

(b) Kutupa mbolea ya wanyama mahali pasiporuhusiwa au kuhifadhi mbolea hiyo katika namna ambayo itasababisha uchafuzi wa mazingira;

(c) Kuosha vyombo vya aina yoyote ya usafiri katika maeneo yasiyoruhusiwa; na

(d) Wamiliki wa Viwanda, kutimua vumbi, moshi, kutiririsha maji machafu, au kutupa taka zinazotoka kiwandani bila kuzingatia kanuni za usafi wa mazingira.

Uhifadhi wa vyanzo vya maji

9. Mtu yeyote hataruhusiwa kujenga au kulima au kufanya shughuli yoyote ya kibinadamu katika maeneo yaliyotengwa kama chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya Binadamu na viumbe hai vingine.

Matumizi ya Vyoo

10. (1) Halmashauri itawajibika kujenga na kuendesha vyoo vya umma kwenye maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

(2) Halmashauri inaweza kuingia ubia na Mtu binafsi, au vikundi au mashirika, au sekta binafsi kujenga na kuendesha vyoo

vya umma (public toilets) katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kwenda haja sehemu ambayo haijatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Ilani ya kuondoa kero

11. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwepo kwa eneo lenye kero ya aina yoyote atamtaka mmiliki wa eneo husika, mpangaji, mtumiaji au mtu yoyote aliyesababisha kero kuiondoa ndani ya muda utakao ainishwa kwenye Ilani kama ilivyoainishwa katika **jedwali la kwanza** sheria ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

## SEHEMU YA TATU
## UTUPAJI TAKA

Uzoaji na utupaji wa Taka

12. (1) Itakuwa wajibu wa kila Mkazi wa Eneo la Jiji kutunza mazingira kwa kutupa taka katika vyombo maalum au maeneo maalum yaliyotengwa kukusanya Taka.

(2) Halmashauri itaanzisha mfumo au utaratibu wa ukusanyaji, uzoaji na utupaji wa taka ambao utashirikisha ngazi za jamii na taasisi mbalimbali katika kuhakisha kunakuwepo mfumo endelevu wa ukusanyaji, uzoaji na utupaji taka Jijini.

(3) Halmashauri itaelimisha Jamii kuhusu kukusanya, kuandaa na kuchakata taka rejea (***Recycling***), taka hatarishi (hazardious), taka zisizooza (inorganic waste) kwenye maeneo yote yanayozalisha taka ili kuzipunguza katika maeneo ya kutupia taka.

Huduma ya Maeneo ya kutupia Taka

13. (1) Halmashauri itatenga, kuanzisha, kujenga na kuendesha maeneo makuu ya kutupa taka *(Sanitary Landfills)* na maeneo ya kutunza taka kwa muda *(Transfer statations).*

(2) Halmashauri inaweza kuingia mkataba na Wakala au mbia kwa ajili ya kujenga na kuendesha maeneo ya kutupia taka.

(3) Halmashauri kwa kushirikiana na Manispaa zitaanzisha na kusimamia vituo vya kukusanya taka *(Collection Points*) na kuweka utaratibu wa uendeshaji.

Uchambuzi wa Taka

14. (1) Taka zote zitachambuliwa kwa makundi ya taka kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(2) Taka zote zitapaswa kuchambuliwa sehemu zinakotoka katika makundi ya taka zenye madhara na zisizo na madhara ili

kuwezesha utofauti katika usimamizi, usafirishaji na utupaji wake.

(3) Taka zote zilizo na madhara zitatunzwa kwenye chombo cha rangi nyekundu kilichowekewa alama ya ***"Taka za hatarishi."***

(4) Taka zote zenye ncha kali zitatunzwa au kuwekwa kwenye mifuko ya pekee na kuwekwa alama ya kutoa tahadhari. ***"Hatari usifungue".***

(5) Taka zote zinazohusiana na taka rejea (***Recycling***) zitachambuliwa na kuwekwa kwenye vyombo maalum vitakavyoelekezwa na Afisa Mwidhiniwa.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa.

15. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa:-

(a) kusimamia uanzishwaji, usimamizi na kushauri kuhusu namna bora ya kutunza na kutupa taka kwa kushirikiana na Mamlaka husika;

(b) Wakati wowote atakaoona unafaa, kuingia katika Jengo au Sehemu yoyote kwa nia ya kukagua uzalishaji na udhibiti wa Taka au kutoa maagizo ya namna ya ukusanyaji, uandaaji na uchakataji wa taka kulingana na aina ya taka;

(c) Kutoa maelekezo namna ya kuhifadhi, kuchambua kutupa au kuharibu taka zilizokusanywa kutoka katika maeneo yote au makazi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wazoa Taka

16. Halmashauri inaweza kuingia Mkataba na Kampuni, Mkandarasi, Kikundi au Wakala ili kufanya shughuli za uzoaji, uondoaji, na usafirishaji wa taka katika maeneo maalum kwa niaba ya Halmashauri.

Uthibiti wa taka katika vyombo vya usafiri.

17. (1) Wamiliki wa Magari au mabasi ya abiria watatakiwa kuweka vyombo maalum kwa ajili ya kuwekea taka zinazozalishwa ndani ya chombo wakati wa safari na kuwataarifu abiria matumizi ya vifaa hivyo;

(2) Mmiliki wa gari au basi la abiria atakuwa na wajibu wa kukusanya na kutupa taka katika eneo lililotengwa kwa ajili ukusanyaji na uzoaji wa taka.

Uhifadhi na Usimamizi wa Taka za Madawa.

18. Taka zote zitokazo vituo vya afya na maduka ya dawa zitahifadhiwa na kuharibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Afya ya Umma ya Mwaka, 2009.

Gharama za utupaji taka

19. (1) Halmashauri itatoza gharama za utupaji taka kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika **Jedwali la Pili** la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoa cheti kitakachoonesha aina na kiwango cha taka kwa mtu, kampuni au Taasisi itakayopeleka taka kwa ajili ya kuharibu.

Zuio la kufanya shughuli katika Dampo

20. (1) Ni marufuku kwa Mtu yeyote, Kampuni au Taasisi au Kikundi kufanya shughuli yeyote katika eneo la Dampo na maeneo yaliyotengwa kuwa Dampo isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Halmashauri.

(2) Si ruhusa kwa mtu yeyote kutoa taka zilizopokelewa Dampo nje ya Dampo isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Halmashauri kitachoonyesha aina, kiasi, matumizi na mahali taka zinapopelekwa.

Marufuku ya kutupa Taka ovyo

21. Ni marufuku:

(a) Kwa Mtu yeyote, Kampuni, Shirika, au yeyote kuzalisha taka na kuzitupa katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya kutupa taka;

(b) Kuteketeza taka kwa kuchoma moto, au kufukia ardhini bila kibali cha Halmashauri;

(c) Kutupa taka kwenye mifereji, mitaro, mito, barabarani, au maeneo ya wazi;

(d) Kutiririsha maji taka kwenye Mifereji, Mitaro, Mito, Barabarani, au Maeneo ya Wazi;

(e) Kufanya biashara au maonyesho ya biashara yeyote au shughuli nyingine yeyote katika maeneo ya karibu au ndani au juu ya Mifereji au Mitaro ya maji, au katika maeneo ya kukusanyia taka, au kwenye Dampo;

(f) Kufanya biashara, kuweka mabango au kufanya shughuli yeyote itakayozuia matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara *(Service road).*

## SEHEMU YA TATU

## UDHIBITI WA UZALISHAJI TAKA ZA VIWANDANI NA HEWA UKAA

Udhibiti wa Uzalishaji Taka

22. (1)Halmashauri itaanda orodha ya wazalishaji wakubwa wa taka kwa ajili ya kuchangia gharama za uanzishaji na uendeshaji wa maeneo ya kutupia taka (Sanitary Landfill).

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa uzalishaji taka kwa kila mmiliki wa kiwanda na mwingizaji wa bidhaa kama ilivyooneshwa katika Kifungu cha ya 8 (1) cha Sheria Ndogo hizi.

(3) Kila anayeingiza au kupitisha mizigo ndani ya Jiji la Dar es Salaam yenye uzito wa tani elfu hamsini kwa Mwezi atalipia shilingi Mia Tano (500/=) kwa Tani.

Udhibiti wa Hewa ya Ukaa

23. (1)Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali itafanya utafiti na uchambuzi ili kutambua viwango mbalimbali vya uzalishaji wa hewa ukaa kutoka katika viwanda na kuchukua hatua pale ambapo kiwango cha uchafuzi kitazidi kile kinachokubalika kisheria.

(2) Halmashauri itashirikiana na wadau wengine kutengeneza mbolea mboji kwa kutumia taka za majumbani, viwandani, sokoni, mimea na maeneo mengine.

(3) Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, Wadau na Makampuni binafsi itafanya, itasimamia na kudhibiti viwango vya uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutoka katika vyombo vya uzalishaji hewa ya Ukaa, vyombo vya moto kama vile mabasi, magari ya mizigo, magari madogo na pikipiki kwa kuvipima viwango vya uchafuzi wa mazingira mara moja kwa Mwaka na kuchukuwa hatua pale ambapo kiwango cha uchafuzi kitazidi kile kinachokubalika kisheria.

Mahusiano na Manispaa kuhusu utekelezaji

24. Halmashauri itaratibu usimamizi wa Sheria Ndogo hizi katika ngazi za Manispaa, Kata na Mitaa.

Makosa

25. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) Atashindwa kutunza au kuweka safi mazingira yanayozunguka Nyumba, Jengo au Sehemu yoyote anayoitumia kwa malazi au biashara au matumizi yeyote ya kibinadamu;

(b) Atashindwa kupanda miti au ataharibu miti au mimea au bustani iliyopandwa kwa namna yeyote;

(c) Atasababisha kero ya kimazingira kwa kutupa taka ovyo au kusababisha kelele kwa sauti kubwa kwa mitambo au muziki au gari au chombo chochote bila kibali cha Halmashauri;

(d) Atatengeneza gari katika eneo la barabara au eneo jingine ambalo halijaainishwa kwa matumizi haya;

(e) Atasababisha moshi usiofaa kwa kuchoma takataka au kitu chochote ambacho kitakuwa kero kwa Watu wengine;

(f) Atatupa taka ya aina yeyote sehemu ambayo si ya kutupa taka;

(g) Atakiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

26. (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au adhabu zote kwa pamoja.

(2) Endapo Mkosaji atakuwa ametenda kosa lililosababisha uharibifu wa mali au miundo mbinu ya usafi, atawajibika kugharamia matengenezo au ununuzi wa miundo mbinu hiyo.

Kufifilisha Makosa

27. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo Mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kukubali kulipa faini kiasi kisichozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) baada ya kujaza fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Pili** la Sheria Ndogo hizi.

Motisha kwa watoa taarifa

28. Halmashauri inaweza kutoa zawadi au motisha ya shilingi Elfu Thelathini (30,000/=) kwa Mtu yeyote atakayewezesha kukamatwa kwa Mtu yeyote atakayetupa takataka ovyo, atakayeharibu bustani, au kukata miti bila kibali maalum cha Halmashauri.

Kufutwa Tangazo la Serikali Na. 31 la tarehe 24/02/2017

29. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo Za (Udhibiti Taka na Utunzaji wa Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mwaka 2017.

## JEDWALI LA KWANZA

## GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA

*(Chini ya kifungu cha ……..)*

| Na. | CHANZO | Ujazo/kipimo | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| 1. | Taka za majumbani zisizochambuliwa | Tani | 5,000/= |
| 2. | Taka za majumbani zilizochambuliwa | Tani | 3,000/= |
| 3. | Taka za Viwandani na sehemu za biashara | Tani | 18,500/= |
| 4. | Kuharibu mali zilizokwisha muda wa matumizi. | Tani | 100,000/= |
| | | Chini ya tani Moja | 90,000/= |
| 5. | Taka zenye madhara isiyo madawa | Kilo | 1,000/= |
| 6. | Taka ya madawa (Red/Blue bag) | Kilo | 4,000/= |
| 7. | Taka za madawa yenye ncha kali na gesi (bio-medical) | Kilo | 5,000/= |
| 8. | Taka za madawa- Vimiminika | Lita | 2,000/= |
| 9. | Taka za magurudumu ya magari baiskeli, piki piki | Kilo | 1,000/= |
| 10. | Taka zinginezo | Tani | 50,000/= |

## JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 27)*

Mimi ……………………………...………mkazi wa Mkoa wa ……………………… nakiri mbele ya …………………….…………..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka 20….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Vyombo vya usafiri na Uboreshaji wa Mapato) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi wa Jiji, Niko tayari kulipa kiasi cha …………………… ninachodaiwa kama faini na hasara niliyosababisha.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU**

Leo tarehe ……………….Mwezi ………………………..Mwaka, ………………

Jina: ………………………………………………. Saini: ……………………….

**Mbele ya**: *(Afisa aliyemkamata mtenda kosa)*

Jina: …………………………………………………. Saini: ……………………….

**TAMKO LA MKURUGENZI**

Kwa mamlaka niliyopewa na Sheria Ndogo nafifilisha kosa lako na kukuamuru Ndugu …………………………………………………….. kulipa faini ya shilingi za kitanzania ……………………………..………………. (Tshs. ………………..) ikiwa ni adhabu kwa mujibu wa kifungu cha …………….. cha Sheria Ndogo hizi TS. Na. ………./20……

Jina: ………………………………………..

Saini: ………………………………………. (*muhuri)*

Cheo: ……………………………………….

**JEDWALI LA TATU**

**ILANI YA KUONDOA KERO**

***(Limetungwa Chini ya kifungu cha 24(1)***

**SEHEMU 'A'**

Ndugu…………………..............wa Mtaa wa………......…… Kata ya……......……… Unataarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……... mwezi……….. mwaka…..... Katika nyumba yako/ eneo lako ya Biashara/ kuishi/ kutolea Huduma /kiwanja* iliyopo eneo la…………………………………..kumekutwa machukizo/kero/uchafu*; kama ifuatavyo;

………………………………….........…………………………………………..
……………………………………….........……………………………………..
……………………………………….........……………………………………..

**SEHEMU 'B'**

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa;

……………….........……………………………………………………………..
……………….........…………………………………………………………….
………………….........…………………………………………………………..

**SEHEMU ‘C’**

Unapewa muda wa siku/ masaa ……………… tangu siku/ saa ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘B’ ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine

…………………………………..

**AFISA MUIDHINIWA**

| **IMETOLEWA NA;** | **IMEPOKELEWA NA;** |
|---|---|
| Jina;……………………….............. | Jina;…………………………………. |
| Saini……………………….............. | Saini………………………………..... |
| Wadhifa…………………................. | Wadhifa…………………………….. |
| Tarehe……………………............... | Tarehe…………………………….... |

*Futa lisilohusika